

Maswali na Majibu

1. Hawa alitengenezwa namna gani?
Hawa alitengenezwa kutoka kwa ubavu uliotolewa kutoka kwa Adamu.
2. Kristo ni mfano wa waume namna gani?
Yeye ni kichwa cha kanisa. Anaipenda na anaijali. Alitoa uhai wake kwa ajili ya kanisa. Mume na awe vivyo kwa mkewe.
3. Kanisa ni mfano kwa wake namna gani?
Kanisa iko chini ya Kristo kama kichwa. Kanisa inapenda Yesu na inamtumikia. Hivi ndivyo mwanamke anastahili awe kwa mumewe.
4. Mwanamume anakaaje?
Ana nguvu na ujasiri
5. Kazi ya mwanamume katika ndoa ni gani?
Anastahili awe kinga kwa mkewe tena amkamilishie mahitaji yake.
6. Mwanamke anakaaje?
Mwanamke ana utu wema, upendo, mtunzaji na wa rehema.
7. Kazi ya mwanamke katika ndoa ni gani?
Analinda boma iwe na nguvu na kulea watoto.
8. Ni vyema kufanya ngono inje ya ndoa?
Hapana. Ni vibaya sana na huwa inaleta shida nyingi.
9. Ni vyema kutalakiana?
Hapana. Ndoa ni mume mmoja na mke mmoja maisha yote.
10. Kitu cha maana sana chenye mume na mke wanatakiwa wafanye mmoja kwa mwingine nini?
Kusaidiana watembee pamoja kwa njia za Mungu mpaka kwa Ufalme wake.

Mistari ya kukariri

Mathayo 19:5 – 6

Waefeso 5:22 – 24

Waefeso 5:25 – 28

Mazungumzo

- ♦ Zungumza juu ya vile mwanamume na mwanamke wanatakiwa wafuate mfano wa Kristo na eklesia.
- ♦ Zungumza juu ya shida zinazoweza kuwoko kukiwa na ngono inje ya ndoa.

Kuandika

Eleza vile Hawa alitengenezwa. Hii ilisababisha uhusiano wa Adamu na Hawa ukawa namna gani?

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 5 Ndoa

SOMA Waefeso 5

SOMO

Mungu alitengeneza Adamu kutoka kwa udongo. Lakini hakutengeneza Hawa kutoka kwa udongo mwingine kama wa Adamu. Mungu alitengeneza Hawa kutoka kwa sehemu ya mwanamume. (Mwanzo 2:21 – 22) Mungu alitengeneza Hawa kutoka ubavu uliotolewa kwa mume. Kwa sababu ya hii, Adamu na Hawa ni mwili mmoja kabisa.

Mungu alipoleta Hawa mbele ya Adamu. Adamu alisema, “Sasa huyu ni mfupa katika mifupa yangu na nyama katika nyama yangu; ataitwa ‘kutoka kwa mume’ mwanamke kwa sababu alitolewa kutoka kwa mwanamume. Kwa hivyo mwanamume atamwaacha baba yake na mama yake na ataambatana na mkewe na watakuwa mwili mmoja.”

Mume na mke wanatakiwa washirikiane kwa kusaidiana wakielekea kwa Ufalme wa Mungu. Hawa alitengenezwa kuwa msaidizi wa Adamu. Mungu hakutoa Hawa kwa kichwa cha mume amtawale. Hakumtoa kwa miguu amganyakie chini. Alimtoa kando yake ili asimame naye kwa kila hali na amsaidie.

Mume na mke ni nyama moja. Ni kama kuwa sehemu mbili lakini ni mwili moja. Sehemu zote za mwili zinashirikiana kwa hisia zao. Sehemu moja ikiwa na maumivu mwili wote utaumia. Tukiwa na afya, mwili wetu wote utasikia sawa. Na hivyo ndivyo ndoa zetu zinatakiwa ziwe. Hawa wenye ndoa wana mwili moja. Mmoja akiwa mgonjwa au hana furaha, mwenzake anatakiwa amhurumie na amsaidie. Mmoja akiwa na furaha, mwenzake naye afurahi na achangamke.


Uhusiano huu wa kipekee ni pamoja na uhusiano wa kimwili kati ya mume na mke – kimwili. Huu uhusiano unatakiwa ulete furaha katikati yao wawili wanaposhirikiana kimwili. Mungu alikusudia uhusiano huu ulete furaha kwa mume na mke. Ni baraka kutoka kwa Mungu - lakini katika ndoa tu. Kila mmoja anatakiwa afurahishe mwenzake.

Mungu alikusudia tuwe na ndoa ili itusaidie pamoja tunapojitahidi kuelekea kwa Ufalme Wake. Uhusiano wa ndani wa kiroho katika ndoa unapea Mungu utukufu wakati wanashirikiana wakisaidiana kwenda kwa Ufalme.

Kristo na kanisa ni mfano wa ndoa 📖 **Soma Waefeso 5:22 – 33.** Uhusiano kati ya Kristo na eklesia ni mfano wa ndoa. Kristo ni kichwa cha eklesia. Kristo alipenda kanisa na akajitoa kwa ajili yake. Kristo anajali eklesia. Anatulinda na anatumia kila siku. Anajua kila hitaji letu. Zaidi sana anatumia kwa mahitaji yetu ya kiroho. Anatusaidia kukua kwa tabia nzuri za Mungu. Anataka sisi tuokoke na tuwe kwa Ufalme waajabu wa Mungu utakaosimamishwa hapa duniani.


Eklesia inapenda Kristo, kwa sababu ametupenda na atatuokoa. Tunajaribu kumtumikia na kutii amri zake. Tunajaribu kufuata mfano wake. Tunajaribu kumpa kila kitu kuonyesha tunampenda.

Katika ndoa ya Kikristo, mume anatakiwa ampende mkewe vile Kristo alipende eklesia. Jambo la maana analotakiwa kufanya ni kumsaidia mkewe ampende na amtumikie Mungu. Anatakiwa awe na haja sana kuliko vitu vingine kwamba mkewe aingie kwa Ufalme wa Mungu. Atajaribu kumpenda na kumjali mkewe vile Kristo anajali eklesia. Kristo hakujaribu kuwa mtawala wala kuchokosa –alipeana uhai wake ajili kwa ya eklesia.



Kristo ni kichwa cha eklesia. Eklesia iko chini ya matakwa ya Kristo. Na vivyo hivyo na mke awe chini ya mume kwa kila jambo. Wanafanya hivyo kama kitendo cha utivu na upendo **kwa Kristo**. Matendo ya wake kwa waume wao yawe kama matendo kwa Kristo.

Katika ndoa ya Kikristo mume na mke wanaonyesha upendo wao kwa Kristo kwa kupendana. Kila mmoja atapenda mwenzake aokoke na awe kwa Ufalme wa Mungu. Wote watasaidiana njiani wakielekea kwa Ufalme.



Mungu amegawia wanaume na wanawake kila mtu vipawa tofauti. Mume ana nguvu na ujasiri, kwa hivyo yeye ni wa kutafuta na kulinda. Mke naye amepewa utu wema, upendo, kutunza na kurehemu. Hivi vipawa vinahitajika kuweka nyumba iwe imara na kulea watoto vizuri. Mume na mke ni lazima wafanye kazi pamoja. Juhudi za mume na za mke zinasaidia nyumba iwe ya nguvu.

Mume mmoja, mke mmoja - maisha yote 📖 **Soma Mathayo 19:4 – 6**

Yesu anatwambia kwamba, ndoa ni kuunganisha watu wawili na wawe wamoja. Mungu alisema ndoa lazima idumu wakati wote wako hai. Aliounganisha Mungu pamoja, mtu mume wala mke asiwatenganishe. Mungu anataka ndoa iwe kuungana mume mmoja na mke mmoja milele.

Wakati mume na mke wanajuana kingono, wanakuwa nyama moja. Mume na mke wawe na ngono. Wasifanye ngono na mtu mwingine yeyote inje. Ngono kati ya mume na mke wake inatakiwa iwe ni baraka kwao wote. Lakini ngono na mtu mwingine ni uovu mkuu sana.

📖 **Soma Mithali 6:27 – 29**

Biblia inasema ngono ni kama moto. Ngono, kama moto, ni kipawa kikubwa kutoka kwa Mungu. Tukiitumia vizuri, inaweza kuleta furaha kubwa kwa ndoa zetu. Ngono kati ya mume na mkewe inaweza kuleta furaha na faraja katikati yao wawili. Lakini ngono inje ya ndoa ni kama moto uziozuliwa. Inavunja ndoa, inaleta watoto haramu na kueneza magonjwa kama ukimwi. Makosa zaidi, wanaokuwa na ngono inje ya ndoa, watakataliwa kuingia kwa Ufalme wa Mungu. Kama moto, ngono inatakiwa kutumiwa vizuri. Mahali tu pazuri pa ngono ni ndani ya ndoa. 1 Wakoritho 6:18 – 20.

Talaka 📖 **Soma Mathayo 5:31 – 32**

Mambo yasipoenda vizuri katika ndoa, inatupasa tuwaombe na tujaribu kuwasaidia waishi kwa amani. Hii sio rahisi kukiwa kunashida. Wanatakiwa usaidizi kutoka kwa Mungu. Kila juhudi lifanyike kuponya hiyo ndoa. Biblia inasema kwamba ni makosa sana kuwa na talaka na kuoja mwingine baada ya kuwa na ndoa. Ndoa ni ya milele.

Tabia kabla ya ndoa 📖 **Soma 1 Wakorintho 6:9 – 11**

Uhusiano wa ngono kabla ya kuoana limekuwa jambo la kawaida kwa nchi nyingi. Watu wenye hawana haja ya kuoana wanatabia ya kuwa na ngono. Hii si tabia ya watu wanaoamini Biblia. Ngono hii inakataswa kwa Biblia. Wawili wakiamua kuoana, Biblia inafundisha kwamba, lazima waongoje mpaka watakapoana ndio wafanye ngono.

Biblia inakataza kutumia ngono vibaya. Ngono kabla ya ndoa, au inje ya ndoa, ukahaba na ushoga ni mambo yanayo kataswa. Ni vizuri kufanya ngono katika ndoa.

Kushiriki kwa baraka za Mungu.

Ndoa iliithinishwa na Mungu. Mume na mke wataendesha ndoa yao vizuri ikiwa wako kwa imani moja. Wanashiriki kwa baraka za Mungu na wanatembea pamoja wakisaidiana kuelekea kwa Ufalme.